

## **Kanisa la Kristo Sio Dhehebu**

(Sehemu ya Nne)

### **Sababu Kumi Na Tatu: Kwa Nini Kanisa La Kristo Sio Dhehebu.**

1. Umadhehebu ni kinyume na Sala ya Bwana katika Yoh. 17:20-21.
2. Umadhehebu ni uasherati wa kiroho, Yoh. 17:20-21.
3. Umadhehebu ni kosa kwa sababu Yesu hajagawanyika, 1 Kor. 1:11-13.
4. Umadhehebu ni kosa kwa sababu Yesu ana mwili moja, sio mingi 1 Kor. 12:13, 20; Efe. 4:4; Kol. 3:15.
5. Umadhehebu unapinga sababu na kusudi ya msalaba, Efe. 2:15-16.
6. Umadhehebu ni kazi ya bure, Mat. 15:9; Zab. 127:1.
7. Umadhehebu unagawanya nyumba za watu, Yoh. 24:15; Amosi 3:3; Marko 3:23.
8. Umadhehebu unapinga ombi la umoja la Paulo, 1 Kor. 1:10.
9. Umadhehebu ni kinyume cha mafundisho ya mitume, Rum. 16:17-18.
10. Umadhehebu ni dhambi ambayo Mungu hapendi, Mith. 6:6-19.
11. Umadhehebu inaonyesha Mungu ni mwandishi wa machafuko, 1 Kor. 14:33.
12. Umadhehebu siyo wa mitume.
13. Umadhehebu itahukumiwa, Marko 3:24-25.

### **Dawa Ya Kupona Madhehebu**

Kama hatutaki umadhehebu ulendeleo tunahitaji wote kurudi kwenye maandiko. Tuache katekismo, kanuni, mawazo ya wanadamu na kufuata kitabu cha Mungu. Leo kama wapo watu wanabishana kwa sababu hawajui saa ngapi. Wakitafuta saa basi watajua muda. Kwa hiyo leo kama tunabishana kuhusu dini ni lazima turudi kwenye Biblia. Biblia tu ina mamlaka leo na Biblia tu inaokoa. Na kama sisi wote ulimwenguni tutafuata Biblia tu basi tutakuwa na “Umoja wa Roho” Efe. 4:1-6.

Pia ni lazima tujue kwamba mbegu inazaa yenyewe. Mbegu ya nyanya haiwezi kuzaa mahindi, Mwa. 1:12. Kwa hiyo kama tunafuata Mbegu ya Neno, Lk. 8:11, hatuwezi kukosa kuwa Kanisa la Agano Jipya. Kwa sababu mbegu ya Neno inazaa Wakristo tu!

Kanisa la Kristo sio dhehebu. Bwana wetu alikuwa bila dhehebu na anatuomba tuwe na umoja katika maneno yake. Kwa hiyo wakati Yesu aliomba kwa Baba yake katika Yoh. 17, alijua tunaweza kuwa na umoja kama tutafuata maneno ya Baba yake. Kwa hiyo kama watu wa Madhehebu wanataka kuponywa leo, ni lazima waache mafundisho yao na kushika maandiko tu!

### **Maswali:**

1. Fafanua neno “Dhehebu” ina maana gani?
2. Toa mifano kutoka Agano Jipya yanayoeleza umoja wa Kanisa.

3. Taja sababu zinzoaeleza Kanisa la Yesu sio Dhehebu.

4. Madhehebu yanatakiwa kufanya nini kama yanataka kuabudu kama mitume walivyoabudu?